

## HALMASHAURI YA WILAYA KIBITI

### MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFAANYIKA OFISI YA DED KIBITI TAREHE 05/11/2021

#### WALIOHUDHURIA

JINA	CHEO	NAFASI
1.0 Denis Kitali	DLNREO	Mwenyekiti
1.0 Rudrick Charles	DPLO	Mjumbe
2.0 Tumainiel.J.Kamnde	HPMU	Katibu
3.0 Arc.Kassim Mponda	DE	Mjumbe
4.0 Salehe Njoma	DLO	Mjumbe
5.0 Anthony Nyange	DCDO	Mjumbe
6.0 Mwl. Zakayo Mlenduka	DEOP	Mjumbe

#### AGENDA YA KWANZA; KUFUNGUA KIKAO

Kaimu Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuwaasa kuwa makini katika kikao. Pia aliwataafu wajumbe kuwa ndugu Denis Kitali – Mwenyekiti amepata udhuru hivyo kawatakia kikao chema

Kikao kilifunguliwa saa 3:22 Asubuhi..

#### AGENDA YA PILI; KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 05/11/2021

Katibu wa kikao aliwasilisha agenda zifuatazo kwa ajili kujadiliwa katika kikao kama ifuatavyo;-

1. Kufungua kikao.

2. Kuridhia Agenda za kikao cha Bodi ya Zabuni cha tarehe 05/11/2021

3. Kupokea na kujadili fedha za UVIKO 19 milioni 460,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa shule shikizi nane (8) ili kuwasaidia wanafunzi wanaoisha mbali na shule mama

4. Kupokea na kujadili fedha za UVIKO 19 **Bilioni** 1,020,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa shule madarasa ya shule za sekondari

5. Kufunga kikao.

## **AGENDA YA PILI; KURIDHIA AGENDA ZA BODI YA ZABUNI ZA TAREHE 05/11/2021**

Mwenyekiti alimualika katibu kuwasilisha Katibu kuwasilisha agenda za kikao cha bodi kisha aliwahoji wajumbe kama wanaridhia agenda hizo kuwa agenda sahihi za kikao hicho. Wajumbe wa Bodi ya zabuni wote kwa pamoja waliridhia agenda hizo kuwa agenda sahihi za kikao hicho.

## **AGENDA YA TATU; KUPOKEA NA KUJADILI BILIONI 1,020,000,000.00 ZA UJENZI WA WA WA VYUMBA VYA MADARASA HAMSINI NA MOJA(51)**

Katibu aliwasilisha taarifa ya ujenzi vyumba vya madarasa 51 kwa shule za sekondari ambazo ni fedha zilizotokana na mapambambano dhidi ya UVIKO 19 yakusaidia kupunguza mlindikano wa wanafunzi darasani na manunuzi haya yatafanyika ngazi ya vituo na kwa njia ya force account .

## **MAONI YA PMU**

PMU ilipokea taarifa ya ujio wa fedha hizo Bilioni 1,020,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa hamsini na moja ili kusaidia mrundikano wa wanafunzi nakuhaidi kusimamia manunuzi hayo kwa mujibu sheria ya ununuzi wa umma.

Baada ya majadiliano wajumbe wa bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Wilaya waliazimia yafuatayo;

## **AZIMIO**

Wajumbe wa bodi ya Zabuni wote kwa pamoja walikubaliana na maoni ya PMU kuwa zoezi la michakato ya manunuzi ya Umma ikiwa ni pamoja na usimamizi wa karibu na kamati zitakazoundwa ili ujenziuanze mara moja ili ujenzi uende kwa kasi na kwa ufanisi mkubwa.


## **AGENDA YA NNE; KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kikao kilifungwa mnamo saa 05.12 asubuhi .

**AGENDA YA TANO; KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kikao kilifungwa mnamo saa 04.01 asubuhi .


**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA;**




.....  
SAINIYA MWENYEKITI



.....  
JINA LA MWENYEKITI



.....  
TAREHE



.....  
SAINI YA KATIBU



.....  
JINA KATIBU



.....  
TAREHE